

## **WANANCHI ACHENI MARA MOJA UVAMIZI WA ARDHI- NAIBU WAZIRI WA ARDHI**

Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Jerry William Slaa, amewataka wananchi kuacha mara moja tabia ya kuvamia maeneo na kumilikishana kiholela badala yake wafuate sheria na taratibu za kumiliki ardhi ili kuepuka migogoro.



Mheshimiwa Slaa ameyasema hayo tarehe 22.09.2023 wakati alipokuwa akizungumza na watumishi wa sekta ya ardhi wa Mkoa wa Morogoro, katika ukumbi wa Mikutano wa Manispaa ya Morogoro, ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya kukagua utekelezaji wa maagizo ya Baraza la Mawaziri ya kuhakikisha Wizara ya Ardhi inatua migogoro ya ardhi inayowakabili wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

“Ni lazima wananchi waache mara moja tabia ya kuvamia maeneo. Sheria za ardhi ziko wazi juu ya njia ya kumiliki ardhi. Kama ardhi ni ya kijiji wapeleke kwenye Ofisi ya kijiji maombi yao ya kumiliki ardhi na kwa ardhi za mijini, hati ya umiliki inatolewa na Kamishna hivyo mwananchi ye yote anayetaka kumiliki ardhi ni lazima afuate sheria za umiliki ili awe salama” alieleza Mheshimiwa Slaa.

Mheshimiwa Slaa pia amewataka wananchi waendeleze maeneo wanayoyamiliki huku akiliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha linawasaidia wananchi ambao maeneo yao yamevamiwa na kusisitiza kwamba dhamana ya kulinda ardhi ya mwananchi haiko mikononi mwa Wizara ya Ardhi bali iko mikononi mwa Jeshi la Polisi hivyo mwananchi ye yote ambaye ardhi yake imevamiwa afike Polisi kwa ajili ya kupata msaada.



Kuhusu suala la utatuzi wa migogoro ya ardhi, Mheshimiwa Slaa amewataka watumishi wa sekta ya ardhi kuhakikisha migogoro yote inatatuliwa ndani ya siku 100 na wanapoitatua wahakikishe wanaweka kwenye maandishi maamuzi waliyoyafikia ili kuwa kama ushahidi endapo mbeleni shida yaweza jitokea.



“Fanyeni kliniki za ardhi kwenye maeneo yenu ili mwafikishie wananchi huduma kwa ukaribu zaidi. Huduma yenu kwa wateja iwe nzuri wanapokuja katika ofisi zenu kutaka huduma. Jitahidini kupunguza malalamiko ya wananchi kwa kutoa huduma kwa weledi. Mkitenda haki mtapunguza malalamiko madogomadogo yanayoweza kujitokeza” aliagiza Slaa

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mheshimiwa Rebecca Nsemwa, amesema, Ofisi yake kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa watawahukumu kwa sheria wavamizi wote wa maeneo ya wakazi wa Morogoro huku akiwataka wananchi wa Morogoro nao kuacha tabia ya kumilikisha kiholela ardhi kwa wageni wanaovamia maeneo yao.



Naye Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Morogoro, ndugu Frank Minzikunte ametaja usimamizi mdogo wa masuala ya ardhi na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu urasimishaji wa ardhi, hasa kwenye uchangiaji wa gharama za urasimishaji kuwa ndio vichochezi vikubwa vya migogoro mingi ya ardhi ndani ya Mkoa wa Morogoro. Hata hivyo ameiomba Wizara ya Ardhi kuongeza bajeti ya ardhi ya Mkoa ili kuongeza nguvu zaidi katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za ardhi ikiwemo upangaji wa mashamba kwa ajili ya kilimo na kutatua migogoro ya ardhi kama vile migogoro baina ya wakulima na wafugaji katika Wilaya za Kilosa na Mvomero.



**MWISHO**